# SILAHA

*ZA*

# VITA VYETU

**PASTOR, TONY OSBORN**

**© August 2024 Pastor Tony Osborn**

Kitabu hiki kimeandikwa na **PASTOR TONY OSBORN**. Haki zote zimehifadhiwa, huruhusiwi kunakili, kurudufu au kutumia sehemu ya kitabu hiki bila idhini ya mwandishi.

Kufanya hivyo itakuwa ni ukiukwaji wa taratibu na hii inaweza kukupelekea kushtakiwa kutoka kwa waandaaji wa kazi hii.

**Pastor, Tony Osborn**

**Dar es salaam, TANZANIA (Afrika Mashariki)**

**Simu: 0762153539/0659085731**

**Instagram / Tiktok: Pastor Tony Osborn**

**ISBN: 978-9912-9873-0-2**

# YALIYOMO


**SHUKRANI. .................................................................... vi**

**UTANGULIZI. ................................................................ viii**

*Sura ya Kwanza*

**MKRISTO ..................................................................... 1**

1.1 Mkristo Aliyeokoka. ............................................... 2

1.2 Tofauti kati ya Mkristo na Mkristo Aliyeokoka. ........... 5

1.3 Safari ya Maisha ya Wokovu. .................................... 24

1.4 Changamoto za Safari ya Maisha ya Wokovu. .......... 25

*Sura ya Pili*

**VITA VYA MKRISTO ..................................................... 37**

2.1 Nini Maana ya Vita?. ................................................ 38

2.2 Vita vya Mkristo ...................................................... 41

2.3 Aina za Vita............................................................. 43

2.4 Kwanini Mkristo anapigwa Vita?.............................. 91

2.5 Je, ni lazima kupigana Vita?...................................... 99

*Sura ya Tatu*

**ADUI TUNAOPIGANA NAO VITA. ............................. 101**

3.1 Adui ni nani?. ......................................................... 102

3.2 Sifa za Adui. ........................................................... 112

3.3 Utamtambuaje adui katika ulimwengu wa mwili?....... 123

3.4 Lengo na Kusudi la adui zetu....................................... 127

3.5 Silaha wanazotumia adui zetu kutupiga. ........................ 139

*Sura ya Nne*

**KUTAMBUA MAJIRA NA NYAKATI TUNAZOKUWA KATIKA VITA. ...................................................................... 161**

4.1 Majira, Nyakati na Muda wa Vita................................. 162

4.2 Utajuaje upo kwenye Vita?........................................... 170

4.3 Nini cha kufanya ukigundua upo kwenye Vita?............ 182

*Sura ya Tano*

**SILAHA ZA VITA VYETU .................................................. 189**

5.1 Silaha ni nini?................................................................ 190

5.2 Silaha tunazotumia kupiga adui zetu............................ 192

5.3 Faida za kutumia silaha mapema.................................. 274

5.4 Hasara za kutotumia silaha mapema............................ 276

5.5 Madhara ya kukimbia na kukwepa vita vyako ............. 279

5.6 Nini kitakufanya ushinde kila vita?.............................. 283

*Sura ya Sita*

**MUONGOZO WA MAOMBI YA VITA............................. 287**

6.1 Maombi ya vita ni nini?................................................ 288

6.2 Maombi ya kurejesha vyote vilivyoibiwa na adui. ......... 289

6.3 Maombi ya kuangusha ngome za adui katika maisha yetu.................................................................. 291

6.4 Maombi ya kung’oa mapando ya adui aliyopanda katika maisha yetu. ....................................................... 293

6.5 Maombi ya kutegua kila mitego waliyotuwekea adui zetu. .................................................................. 295
6.6 Maombi ya kufuta na kuharibu kila mipango ya adui katika maisha yetu............................................ 297
6.7 Maombi ya kurudisha mashambulizi kwa adui zetu. .... 298
6.8 Maombi ya kufungua kila kifungo alichoweka adui katika maisha yetu......................................................... 300
6.9 Maombi ya kufukua vitu vyetu vilivyozikwa na adui. ... 302
6.10 Maombi ya kuwatoboa macho adui zako ili wasikuone wakiwa wanafanya uchawi wao................. 303
6.11 Maombi ya kuondoa mipaka aliyokuwekea adui na kuondoa roho ya kucheleweshwa. .............................. 306
6.12 Maombi ya ulinzi na shukrani. .........................307

**HITIMISHO ........................................................................ 308**

**MAELEKEZO NAMNA YA KUTUMA SADAKA YAKO NA KUJIUNGA NA PARTNERSHIP.................. 310**

# SHUKRANI

Ninamshukuru Mungu sana kwa uaminifu wake na kwa kunijalia ROHO MTAKATIFU ambaye kwa mafunuo na hekima kubwa ameniwezesha kukiandika kitabu hiki kuanzia mwanzo mpaka mwisho na kwa kadri ya wingi wa hekima na maarifa yake kitabu hiki kikakamilika.

Siri zilizoandikwa humu kwa uwezo wa Roho wa Mungu zitakusaidia na kukuongoza na kukuonyesha nini unapaswa kufanya unapokutana na vita katika maisha yako na ni silaha gani wewe kama mkristo unatakiwa uzitumie kupigana vita vyako iwe katika ulimwengu wa Roho au ulimwengu wa damu na nyama.

Neno la Mungu linasema katika kitabu cha;

**Waefeso 6:10-13**

**"Hatimaye, mzidi kuwa hodari katika Bwana na katika uweza wa nguvu zake. Vaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kuzipinga hila za Shetani. Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama; bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho. Kwa sababu hiyo twaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kushindana siku ya uovu, na mkiisha kuyatimiza yote, kusimama."**

Neno hili linatuonyesha ya kuwa ili kushinda vita sisi kama wakristo zipo silaha ambazo tunatakiwa kuzitumia na kitabu hiki kitakueleza kwa undani zaidi juu ya silaha hizo na namna ya kuzitumia ili kupata ushindi.

Shukrani zangu za pekee ziwafikie watoto wangu wa kiroho wote, ndani na nje ya nchi ya Tanzania, kwa kunipenda, kuniombea na zaidi ya yote kunipokea na kuniamini, kumuamini Mungu aliyeniita na huduma iliyopo ndani yangu.

Ninawashukuru sana kwa kuwa nyie mmenipa nafasi katika mioyo yenu na kuamini kile kitu na huduma Mungu ameweka ndani yangu.

Ninawapenda, ninawaombea na Mungu wa mbinguni awabariki sana.

Kiupekee kabisa ninamshukuru mke wangu mpenzi Mrs Neema Tony Kapola ambaye amekuwa akikesha pamoja nami, akisukuma na kusimamia kwa ufasaha ukamilifu wa kitabu hiki. Ninakupenda na asante kwa kusimama na mimi katika wito na kazi hii ambayo Mungu amenipa.

Mungu aendelee kukuonekania wewe na familia yako ndani ya mwaka huu.

*Amen……………………*

***~Pastor Tony Osborn***

# UTANGULIZI

Kitabu hiki cha **"SILAHA ZA VITA VYETU"** ni kitabu ambacho kimelenga kumfundisha na kumpa maarifa na hekima mkristo juu ya silaha za kutumia nyakati ambapo atakutana na vita au mashambulizi kutoka kwa adui shetani au adui wanaotuzunguka katika maisha yetu.

Maisha yetu yamezungukwa na maadui pande zote na hii ni kwa watu wote iwe ameokoka au hajaokoka, iwe anamjua Mungu au hamjui Mungu. Maadamu wewe ni binadamu uliyeumbwa na Mungu, utakutana na vita tu. Katika biashara utakutana na vita vyake, katika mahusiano na ndoa utakutana na vita vyake, katika elimu na kazi utakutana na vita vyake, katika siasa nako utakutana na vita vyake na hata katika utumishi na huduma nako utakutana na vita vyake. Kwa hiyo , kiufupi kabisa ni kuwa hakuna eneo lolote utakalokuwepo katika maisha yako ambapo hutokutana na vita.

Sasa ili uwe mshindi katika hilo eneo ni lazima uwe na ufahamu juu ya;

- ❖ Vita unayopigana (Ni lazima ujue sababu nyuma ya vita unayopigwa, hii itakusaidia sana katika kupigana vita vyako kwa akili na ufahamu.)

- ❖ Silaha anazotumia adui kupigana na wewe (Ni lazima pia uwe na ufahamu wa kutosha juu ya silaha na njia ambazo adui anatumia ili kupigana vita na wewe, ukijua silaha za adui na wewe utajua kwa wakati huu utumie silaha gani ili kumshinda.)

- ❖ Silaha gani utumie na kwa wakati upi ili umshinde adui yako (Wewe pia unatakiwa ujue ni silaha zipi utatumia ili kuweza kupigana na kumshinda adui yako).

Haya ni mambo ya msingi ambayo unatakiwa uyazingatie ili kuweza kushinda vita zote ambazo utakutana nazo katika maisha yako.

Hiki kitabu ni kitabu ambacho ndani yake utajifunza juu ya vita na ni kwanini unapigwa vita lakini utajifunza juu ya aina za vita ambazo utakutana nazo katika maisha yako na silaha za kutumia ambazo zitakuwezesha kupigana vita na kushinda.

Mwisho kabisa nimekuwekea muongozo wa maombi ya vita ambayo yatakusaidia kukuongoza kuomba hata kwako wewe ambaye umeokoka hivi karibuni na bado hujui kuomba vizuri. Kwa kutumia maombi hayo utaweza kuomba na kuamrisha adui aachilie milki zako na vyote vilivyo vyako kwa jina la Yesu.

Zaidi ya yote kitabu hiki kitakuwa msaada wako wa karibu siku zote ambapo utakuwa unakutana na vita. Kila mara utakapokuwa unakutana na vita hakikisha unachukua kitabu hiki na kufanya maombi yaliyomo humu na utaona namna ambavyo yatakuletea matokeo.

Neno la Mungu linasema katika kitabu cha;

**Yeremia 51:20**

**"Wewe ni rungu langu na silaha zangu za vita; kwa wewe nitawavunjavunja mataifa; na kwa wewe nitaharibu falme."**

Kwa hiyo usiogope kupigana vita mwanangu maana Mungu mwenyewe ataingia vitani na wewe na kukusaidia kushinda vita zote kwa jina la Yesu.

***~Pastor Tony Osborn***

# 1

*Sura ya Kwanza*

# MKRISTO

**"Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake; waliozaliwa, si kwa damu, wala si kwa mapenzi ya mwili, wala si kwa mapenzi ya mtu, bali kwa Mungu."**

**Yohana 1:12-13**

## 1.1 MKRISTO ALIYEOKOKA

Safari yetu ya kusoma na kukielewa kitabu hiki inaanzia katika maisha halisi ya mkristo mwenyewe.

### *Mkristo ni nani?*

Mkristo ni yule mtu ambaye ni mshirika wa dini ya kikristo na ni mtu ambaye anaamini juu ya uwepo wa Kristo na kuwa alikuja duniani katika umbo la mwanadamu na kuteswa na kufa kwa ajili ya dhambi za ulimwengu mzima.

Wakristo wengi ni watu ambao wanaendesha maisha yao katika misingi ya dini za kikristo walizokulia au walizozikuta kwa wazazi wao.

### *Mkristo aliyeokoka ni nani?*

Mkristo aliyeokoka (mlokole) ni yule ambaye haishii tu katika kuamini uwepo wa Yesu ila pia ameamua kumwacha huyo Yesu anayemwamini kuwa Bwana na mwokozi wa maisha yake. Tunavyosema kuwa Yesu anakuwa Bwana wa maisha yetu maana yake ni kuwa Yesu anakuwa kiongozi mkuu wa maisha yetu na yeye ndio mfanyaji maamuzi mkuu katika maisha yetu, kiufupi zaidi ni kuwa ***"Yeye ndie anayeishi na sio sisi tunaoishi."*** Hivyo huyu mtu ataenenda na kutenda kama vile Yesu anavyotaka na sio kama dini au wazazi wanavyotaka.

**Wagalatia 2:20**

**"Nimesulubiwa pamoja na Kristo, wala si mimi tena ninayeishi, bali Kristo ndiye aishiye ndani yangu. Uhai nilio nao sasa katika mwili, ninaishi kwa imani ya mwana wa Mungu, aliyenipenda na kujitoa kwa ajili yangu."**

Kwa hiyo Mkristo aliyeokoka ni yule ambaye anamfuata Yesu sio kwa sababu ya wazazi wake, na wala sio kwa sababu za kidini ila ni yule mtu ambaye amefanya maamuzi kwa akili zake mwenyewe na kumpokea Yesu kuwa Bwana na mwokozi wa maisha yake.

Wengi huwa wanaamini kuwa kuokoka ni dini mpya lakini sio kweli bali kuokoka (wokovu) ni mpango kamili wa Mungu mwenyewe wa kutafuta kile kilichopotea (mwanadamu aliyepotea katika dhambi) na kisha kumtoa mwana wake wa pekee Yesu ili afe kwa ajili yao. Kwa hiyo kuokoka sio dini kama wengi wanavyojua, kuokoka ni maamuzi ya mtu binafsi ya kuamini na kufata kile ambacho Mungu amekichagua kuwa kama njia ya kuokolewa kwa binadamu wote. Na ndio maana watu wakiwa wanaokoka huwa wanaulizwa; Je, umekubali kumpa Yesu maisha yako? Hii ikimaanisha kuwa ni swala la mtu mwenyewe kuamua. Hizi dini zote unazoziona lengo lake ni moja tu nalo ni kumtafuta Mungu na ndio maana zipo nyingi na kila moja ikiwa na sheria na kanuni zake, ila likija swala la Mungu kuokoa wanadamu njia ni moja tu Yesu Kristo.

**Matendo ya Mitume 4:10-12**

**"Ijulikane kwenu nyote na kwa watu wote wa Israeli kwamba: Ni kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti, ambaye ninyi mlimsulubisha lakini Mungu akamfufua kutoka kwa wafu, kwa jina hilo mtu huyu anasimama mbele yenu akiwa mzima kabisa.** Huyu ndiye **"jiwe ambalo ninyi wajenzi mlilikataa, ambalo limekuwa jiwe kuu la pembeni."**

**Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hakuna jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo."**

Ni kwa njia ya wokovu tu sisi binadamu wote tunaokolewa na jina pekee tulilopewa wanadamu wote kuokolewa nalo ni Yesu tu na sio jina jingine.

Jina jingine? Lakini watu wengi wanalo jina Yesu (Yeshua au Yoshua Kiebrania) jina hilo maana yake ni nini? Ili unaposema umeokolewa kwa jina la Yesu angalau ujue maana yake ni nini.

**Mathayo 1:21**

**[21]Naye atazaa mwana, nawe utamwita jina lake Yesu, maana, yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao.**

Jina lake Yesu… **maana, yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao.**

Neno la Kiyunani la jina katika ***Matendo 4:12*** ni ***onoma*** ambalo linamaanisha (mamlaka, tabia au sifa au kazi ya mtu).

Kwa hiyo jina la Yesu siyo herufi bali ni **mamlaka, tabia au sifa au kazi yake katika kuokoa.**

**Ni mamlaka, tabia au sifa au kazi gani ya Yesu unaamini ili upate kupokea wokovu wake?.**

**Warumi 10:9**

**[9] Kwa sababu, UKIMKIRI Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka.**

Ukiangalia kwenye lugha ya asili ya Kigiriki ni HOMOLOGEO ikiwa na maneno mawili HOMO ikiwa na maana ya MOJA AU KUFANANA na LOGOS ikiwa na maana ya KUSEMA/ KUTAMKA/ KUKUBALI/ KUWAZA.

Kwa hiyo ni sawa na kusema;

…Pande zaidi ya moja kukubaliana.

... Kukiri sawa na…

... kutamka sawa na...

... kuwaza sawa na...

Au KUWA KATIKA MAKUBALIANO.

**Waefeso 2:8-9**

**[8] Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu;**

**[9] wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu.**

Wokovu ni zao la Imani. Kuweka Imani yako katika kazi ya Kristo. Yaani kuwa alikufa na kufufuka kwa ajili ya dhambi zako. Hakuna jina jingine wala njia nyingine. Huyu ndiye aliyeokoka.

Kwa hiyo sehemu kubwa ya kitabu hiki tutamuongelea huyu mkristo aliyeokoka ambaye yeye binafsi ameamua kumwamini Yesu na kumruhusu kuwa Bwana na mwokozi wa maisha yake. Huyu ndio mkristo ambaye huwa anapigwa sana vita kuliko viumbe na pengine kuliko watu wote hapa duniani.

Sasa kabla ya kujifunza juu ya safari halisi ya maisha ya mkristo, tuangalie tofauti kati ya mkristo wa kawaida na mkristo aliyeokoka.

## 1.2 TOFAUTI KATI YA MKRISTO NA MKRISTO ALIYEOKOKA

Kuna tofauti kubwa sana kati ya mkristo wa kawaida na mkristo aliyeokoka ijapokuwa wote wanaamini katika Yesu. Tofauti zao kubwa zipo katika mambo haya yafuatayo.

**i. Ufahamu juu ya Mungu.**

Tofauti ya kwanza inayomtofautisha mkristo wa kawaida na yule aliyeokoka ni ufahamu wao juu ya Mungu. Wakristo wengi wa kawaida huwa wana ufahamu mchache kumhusu Mungu wao. Ni watu ambao wanapenda kuambiwa mambo ya kumhusu Mungu wao ila wao binafsi hawaweki juhudi ya kumjua huyu Mungu wao. Kwa hiyo wao wanamjua Mungu kwa kiasi kidogo tu cha wanachosikia au kuambiwa.

Wakristo waliookoka ni wale ambao huwa wana ufahamu wa kutosha kuhusu Mungu wao na huwa wanapenda kujifunza na kutaka kumjua Mungu wao na kumuelewa. Kwa hiyo hawaishii tu pale wanapoambiwa kuwa "Mungu huwa anafanya njia pasipo na njia" bali wanatamani kumjua na kumuona huyo Mungu katika maisha yao akifanya njia kweli.

**Danieli 11:32**

**"Na wao wafanyao maovu juu ya hilo agano atawapotosha kwa maneno ya kujipendekeza; lakini watu wamjuao Mungu wao watakuwa hodari, na kutenda mambo makuu."**

Neno limetuelezea vizuri kabisa hapo juu ya kuwa; wale wanaomjua Mungu wao watakuwa hodari na kutenda mambo makuu. Kamwe huwezi kujiamini katika kufanya mambo makubwa kama huna imani na kama humjui Mungu wako.

*Sasa ufahamu juu ya Mungu tunautazama katika namna zipi?*

Kujua tu kuwa kuna Mungu haitoshi na wewe utasema kuwa unamjua Mungu kama utayajua mambo makuu yafuatayo kumuhusu.

- ❖ Kujua na kufahamu sauti yake.